

# Kwa Nini Wenye Ukoma Walitaka Kuponywa

Ukoma unatajwa mara nyingi katika Biblia. (2 Wafalme 5:1; Luka 5:12-14) Ukoma ulikuwa ugonjwa wa aina gani? Kwa nini wenye ukoma walitamani sana kuponywa?

Mkiwa familia, jifunzeni mengi kuhusu ugonjwa huo ambao Biblia huuita ukoma. Mnaweza kuchunguza kitabu *Insight on the Scriptures* (ambacho kinapatikana pia katika lugha nyingi kwenye [jw.org](http://www.jw.org) chini ya PUBLICATIONS > ONLINE LIBRARY) au machapisho mengine mnayoweza kupata.

Waisraeli waliopona ukoma walipaswa kufuata utaratibu fulani kabla ya kurudia maisha yao ya kawaida. Someni Mambo ya Walawi 14:2, 4, 8, 10, 20, na kisha mpange picha zilizo hapo chini katika mpangilio ambao ulifuatwa na mtu aliyeponywa ukoma na pia kuhani.



- **SASA JARIBU KUFANYA HIVI:** Someni Luka 5: 12-15 na mjifunze jinsi Yesu alivyowajali watu wenye ukoma aliokutana nao. Kisha, andikeni orodha ya watu wagonjwa sana mnaojua. Zungumzieni jinsi mnavyoweza kumwiga Yesu na kuwaonyesha fadhili.

**Majibu:** 1. Mtu aliyepona ukoma aletwa kwa kuhani. 2. Mtu mwenye ukoma apeleka ndege wawili. 3. Mtu mwenye ukoma anataa mavazi yake. 4. Mtu mwenye ukoma apeleka kondoo dume wawili na mwana-kondoo jike mmoja. 5. Kuhani anataa matoleo.